Taarifa kwa Vyombo vya Habari | 15 Februari 2022

Wananchi na viongozi wa kijamii huko Pangani wanafanya kazi pamoja kuleta mabadiliko

Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuongezeka kwa ushiriki wa wananchi kwenye mikutano ya vijiji, kutungwa kwa sheria ndogondogo zenye tija kwa wananchi, agenda za wananchi kupewa kipaumbele na uboreshaji wa utoaji huduma.

15 Februari 2022, Pangani: Twaweza inafanya kazi na Pangani Coast Paralegal (PACOPA), mamlaka ya serikali za mitaa na wakazi wa Pangani kuboresha ushirikiano kati ya wananchi na mamlaka mbalimbali ili kwa pamoja waweze kuboresha huduma, kuimarisha uwezo wa serikali za mitaa na kuboresha ushiriki wa wananchi.

Haya yote yamewezekana kupitia matumizi ya mbinu shirikishi kama vile uandaaji wa filamu shirikishi zenye picha elimishi, maigizo pamoja na maonesho kwa ajili ya maendeleo. Twaweza na PACOPA kwa pamoja waliwabaini na kuwapa mafunzo wananchi wenye ari ya mabadiliko ndani ya jamii, kufanya utafiti shirikishi kupitia filamu na tamthilia, na kuandaa na kutekeleza kwa pamoja mipango kazi ya kushughulikia masuala yaliyoibuliwa. Pia Twaweza ilifanya utafiti wa kina ili kuelewa mazingira na hali halisi ya ushiriki wa wananchi na huduma za jamii kwenye wilaya ya Pangani.

Matokeo muhimu ya utafiti ni pamoja na:

- Wakazi 3 kati ya 10 wa Pangani (29%) wako kwenye kikundi mojawapo cha kijamii kama vikundi vya mikopo au vya maendeleo
- Wakazi wa Pangani 6 kati ya 10 wanafahamu mikutano ya kijiji iliyofanyika kipindi cha miezi 12 iliyopita na kati yao 7 kati ya 10 wanasema wamehudhuria mikutano hii. Hata hivyo, majadiliano ya kina katika vikundi na mapitio ya daftari la mahudhurio vinaonesha mahudhurio yalikuwa chini zaidi.
- Baadhi ya wakazi wanaohudhuria mikutano hiyo, wanasema hawaridhishwi nayo kwasababu hawaoni kama masuala yao ya kipaumbele yanashughulikiwa, pia hawapati mrejesho kutoka serikali za mitaa kuhusu utekelezaji wa masuala yaliyoibuliwa siku za nyuma.
- Wananchi wana uwezekano mkubwa wa kuwasiliana na viongozi wa vijiji kuliko wabunge au watendaji wa kata. Hata hivyo, nusu ya wakazi wa Pangani (49%) wanasema hawajawahi kuwasiliana na mwenyekiti wao wa kijiji.
- Wakazi wa Pangani wanapenda zaidi kuchangia maendeleo ya jamii yao kupitia kutoa nguvu kazi (34%) au kuchangia vifaa vingine(30%) kuliko michango ya fedha (23%).
- Mamlaka za mitaa za Pangani zinaona Pangani ina upungufu wa wafanyakazi, waliopo hawathaminiwi na hawana na rasilimali za kutosha kuwawezesha kutekeleza majukumu yao ipasavyo.
- Wakazi 8 kati ya 10 wa Pangani(78%) waliripoti kuwa bajeti na taarifa za matumizi hutolewa kwa wananchi wakati wa mikutano ya Halmashauri ya Kijiji.
- Wakazi 2 hadi 4 kati ya 10 hawaridhishwi kabisa na utoaji wa huduma. Wananchi hawafurahishwi zaidi na uduni wa huduma za: usafiri na miundombinu, huduma za afya, na upatikanaji wa umeme. Wananchi wameridhishwa kidogo na elimu, na wamegawanyika kuhusu kuridhishwa na huduma za maji.

Hadi sasa, masuala kadhaa yaliyoibuliwa kupitia utafiti shirikishi na zoezi la pamoja la kupanga vipaumbele vya changamoto zilizoibuliwa na makundi mbalimbali, yamepatiwa ufumbuzi.

Kule Msaraza

- Mgogoro wa muda mrefu wa kuhusu kisima cha maji huko Bushiri umepatiwa ufumbuzi kupitia mkutano wa hadhara na majadiliano ambayo yalipelekea mamlaka ya maji ya eneo hilo kupunguza bei ya maji, na kuwawezesha wananchi kutumia vyanzo vya maji ambavyo vinapatikana kwa urahisi na karibu yao. Migogoro ya

vyanzo vya maji hasa kati ya watumiaji mbalimbali ni ya kawaida kote nchini na utatuzi wa Msaraza unaweza kuwa mfano wa kuigwa na hamasa kwa wengine.

- Wananchi walibaini uhusiano mbaya kati yao na viongozi wa mitaa kuwa ni tatizo jingine kubwa. Mikutano imefanyika kila kitongoji kujadili masuala hayo, na ushiriki wa wananchi kwenye mikutano ya kijiji sasa umeimarika kutoka wastani wa watu 50 wanaohudhuria hadi 100.
- Wakazi walilalamikia ulevi wa kupindukia ndani ya jamii yao, na kukosekana kwa sheria zinazozuia uuzaji holela wa pombe kwenye maeneo ya makazi. Mamlaka za mitaa zilishiriki katika kutatua kero hiyo kwa kutenga eneo rasmi ambalo pombe itauzwa, pia ilitunga sheria ndogo ndogo kudhibiti hali hiyo.
- Pia Wakazi wa Msaraza waliona wana changamoto ya jinsi watoto wanavyolelewa katika jamii yao. Mamlaka za mitaa ziliandaa mpango wa kuwafikia wazazi ili kuwaongezea ujuzi na maarifa na kutunga sheria ndogo ndogo za kuzuia watoto wenye umri mdogo kuhudhuria matukio ya kijamii usiku. Sheria hiyo pia inatoa adhabu kwa wazazi ambao watoto wao watabainika kukiuka sheria hizo.

Kule Mkwaja

- Wananchi walikuwa na matatizo makubwa ya upatikanaji wa maji safi na salama. Visima vingi havina mifuniko na matokeo yake wakazi walikuwa wakikuta takataka katika visima wanapochota maji. Aidha, visima vilikuwa vikichimbwa bila kuzingatia viwango kubalifu, mfano visima vingi vilikuwa karibu na mashimo ya vyoo na hivyo kuhatarisha afaya za wakazi wa Mkwaja. Mamlaka za mitaa zimefanikiwa kukarabati visima vinane na kutengeneza mifuniko na sasa wametenga bajeti ya kuboresha visima vingine 10. Pia wamewaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa maji safi na salama.

Kule Mwera

- Changamoto kadhaa zilibainika ikiwemo uhaba wa maji na miundombinu mibovu, mahusiano duni kati ya viongozi na wananchi, taarifa za bajeti na matumizi ya serikali za mitaa hazitolewi kwa wananchi mara kwa mara, ukatili dhidi ya watoto, matatizo katika sekta ya afya ikiwemo uhaba wa dawa na watumishi; na rushwa.
- Hadi sasa mafanikio makubwa ni viongozi wa mitaa kukubali kutoa taarifa za bajeti na matumizi sekta ya maji ili wananchi waone jinsi fedha zinavyotumika na kuwafanya wawe tayari kuchangia katika kuboresha sekta hiyo.

Ili kupata mafanikio haya mapema na kuhakikisha mahusiano bora kati ya wananchi na serikali yao yanaendelea, Twaweza itaendelea kutoa ushauri elekezi katika utekelezaji wa mpango kazi wa waliojiwekea wananchi na viongozi wao.

Aidan Eyakuze, Mkurugenzi Mtendaji wa Twaweza, alisema *"Mpango huu ni ukumbusho kwetu kwamba ili maendeleo yaweze kutokea, tunatakiwa kuwashirikisha wananchi na kuhakikisha wanashirikiana na viongozi wao. Wananchi na viongozi wanapoaminiana na kumuona mwingine kama mdau na mshirika, taarifa zinapotolewa kwa pande zote mbili kwa uhuru na kwa wakati, na pale ambapo wote wana hamasa, ari, uwezo na fursa za kufanya kazi pamoja, matokeo yake ni mafanikio ya wazi na ya haraka. Tunaamini fikra hizi zinaweza kuingizwa kwenye dira ya utawala wa awamu ya sita ili kuleta maendeleo ya kweli na mabadiliko ya nchi yetu."*

---- Mwisho ----

Kwa taarifa zaidi:
Annastazia Rugaba | e: arugaba@twaweza.org | t: (+255)(0)687 22 197

Maelezo kwa Wahariri

- Muhtasari na takwimu husika zinapatikana hapa www.twaweza.org,
- Twaweza inafanya kazi kupitia tafiti, ushahidi na kuchua hatua ili kuonesha jinsi ambavyo wananchi wanavyoweza kushirikiana kutatua matatizo yao na kuifanya serikali iwajibike vizuri zaidi kwa wananchi; kuwezesha wananchi kupaza sauti zao kwenye masuala yanayohusu maslahi na uzoefu wao ili yasikilizwe na yachukuliwe kwa uzito wakati wa kufanya maamuzi; na inahimiza kuweka mazingira wezeshi kwa ushirikishwaji wa wananchi na serikali kuitikia mahitaji ya wananchi nchini Tanzania, Kenya na Uganda. Tufuatilie kwenye Twaweza Tanzania (Facebook), @Twaweza_NiSisi (Twitter), Twaweza East Africa (Instagram).